



Taarifa kwa waandishi wa habari

24 Novemba 2016

## **Wananchi wanasema ubora wa elimu umeongezeka tangu kuanzishwa kwa mfumo wa elimu bila malipo ya ada**

**Lakini Watanzania 6 kati ya 10 wangewapeleka watoto wao shule binafsi kama wangekuwa na uwezo**

**24 Novemba 2016, Dar es Salaam:** Kufuatia kuanzishwa kwa mfumo wa elimu bila malipo ya ada, asilimia 50 ya wananchi wanasema ubora wa elimu umeongezeka. Lakini asilimia 35 wanasema ubora wa elimu umebakira palepale huku asilimia 15 wakisema umeshuka.

Matokeo haya yametolewa na Twaweza katika muhtasari wake *Hali halisi: Maoni ya wananchi juu ya elimu bila malipo ya ada*. Muhtasari huo unatokana na takwimu kutoka *Sauti za Wananchi*, utafiti wa kwanza barani Afrika wenye uwakilishi wa kitaifa na unaotumia simu za mikononi. Matokeo haya yanatokana na takwimu zilizokusanywa kutoka kwa wahojiva 1,806 kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara kati ya tarehe 7 na tarehe 14 agosti 2016. (Zanzibar haihusiki kwenye matokeo haya)

Wananchi wengi wana mitazamo chanya juu ya elimu nchini Tanzania, lakini, ni dhahiri kuwa shule za serikali bado zinakabiliwa na changamoto mbalimbali. Kwa mujibu wa wahojiva, changamoto kuu ni ukosefu wa walimu (imetajwa na asilimia 34), madawati (asilimia 30) na madarasa (asilimia 13), pamoja na uhaba wa vitabu (asilimia 7).

Kwenye kaya 8 kati ya 10 zenye watoto, asilimia 90 ya watoto hao husoma katika shule za serikali. Hata hivyo, iwapo shule za serikali na binafsi zote zingekuwa bure, wananchi 6 kati ya 10 wanasema wangewapeleka watoto wao katika shule hizo. Hii ni ishara ya kuwa wananchi wana mashaka na ubora wa elimu kwenye shule za serikali. Wananchi walitaja elimu bora (asilimia 45), uwepo wa walimu wanaofanya kazi kwa bidii na wanaopewa motisha (asilimia 12), pamoja na idadi ya kutosha ya walimu (asilimia 12) kama sababu kuu za kuzipendelea shule binafsi.

Wananchi wengi walisema elimu ni bora katika shule binafsi za msingi (asilimia 51) na sekondari (asilimia 56). Hii ilitofautiana sana na wale waliosema shule za msingi (asilimia 22) na sekondari (asilimia 19) za serikali zina ubora.

Asilimia 85 ya wananchi walisema kwamba kutokujihusisha kwa wazazi kwenye masuala ya shule ni changamoto kuu kwenye elimu. Changamoto zingine zilizotajwa ziliikuwa ni pamoja na miundombinu ya shule (imetajwa na asilimia 83), matokeo mabaya ya wanafunzi (asilimia 83), nidhamu ya wanafunzi (asilimia 79), kutowapa motisha walimu (asilimia 66), na ubora wa mtaala (asilimia 62).

Kutokujihusisha kwa wazazi kwenye masuala yahusuyo shule kunadhahirika katika idadi ya wazazi ambao hawajawahi kutoa msaada wowote kwenye shule za watoto wao (asilimia 88). Pia, wazazi walioikutana na walimu wa watoto wao mara moja au mbili kwa mwaka ni asilimia 52 na wazazi walitembelea shule wanazosoma watoto wao mara moja au mbili ni asilimia 57 katika mwaka uliopita.

*“Miezi kumi na miwili iliyopita, asilimia 76 ya wananchi walikuwa na matarajio makubwa sera ya elimu bila malipo ya ada itaboresha elimu. Leo hii, nusu ya wananchi wanasema ubora wa elimu umeongezeka,”* anasema Mkurugenzi Mtendaji wa Twaweza, Aidan Eyakuze. *“Ni vema tukajiuliza, je, mafanikio ya kampeni maarufu ya kupata madawati yanalinganishwa na uboreshaji wa elimu? Je, wakati sera mpya inatekelezwa, mchango wa wazazi na walezi kuboresha elimu unachukua sura ipi? Je, matokeo ya wanafunzi kuanzia mwaka 2016 yatadhihirisha ubora unaotarajiwa? Ni vema tukaendelea kuyajadili maswali kama haya kwa maufaa ya watoto na vijana wetu.”*

---- **Mwisho** ----

**Kwa taarifa zaidi wasiliana na:**

Risha Chande, Mshauri Mwandamizi wa Mawasiliano, Twaweza

**Barua pepe:** [rchande@twaweza.org](mailto:rchande@twaweza.org) | **Simu:** (+255) (0) 656 657 559

**Maelezo kwa Wahariri**

- Muhtasari huu na takwimu zake zinapatikana kupitia [www.twaweza.org](http://www.twaweza.org), au [www.twaweza.org/sauti](http://www.twaweza.org/sauti)
- Twaweza inafanya kazi ya kupima uwezo wa watoto kujifunza, wananchi kuwa na utayari wa kuleta mabadiliko na serikali kuwa wazi na sikivu zaidi katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda. Twaweza ina programu, wafanyakazi na ofisi katika nchi zote tatu, na utaratibu unaoheshimika kimataifa wa kujifunza, ufuatiliaji na tathmini. Programu zetu muhimu ni pamoja na Uwezo, ambayo ni tathmini kubwa ya kila mwaka ya wananchi barani Afrika inayopima viwango vya watoto vya kujifunza kwenye maelfu ya kaya, na *Sauti za Wananchi*, utafiti wa kwanza Afrika wenyewe uwakilishi wa kitaifa unaofanyika kwa njia ya simu ya mkononi. Pia tunashiriki kwenye masuala ya umma na sera, kupitia ubia wetu na vyombo vya habari, juhudhi za kimataifa zinazoshughulikia masuala ya uongozi kama vile mpango wa Ushirikiano na Serikali wazi (OGP).
- **Tovuti:** [www.twaweza.org](http://www.twaweza.org) **Facebook:** Twaweza Tanzania **Twita:** @Twaweza\_NiSisi